

HALMASHAURI YA MJI KIBAHA
Barua zote zipelekwe kwa mkurugenzi wa mji

S.L.P 30112
SIMU Na: 023 - 2402886
FAX Na: 023 – 240 2007



OFISI YA MKURUGENZI
MJI WA KIBAHA

TAARIFA KWA UMMA

HALI YA UFAULU KWENYE MITIHANI YA KITAIFA YA KIDATO CHA IV, KIDATO CHA II,
DARASA LA VII NA DARASA LA IV HALMASHAURI YA MJI KIBAHA, 2020

Kibaha, 10 Machi, 2021

Katika matokeo ya mitihani ya kitaifa yaliyotangazwa Januari 15, 2021 na Katibu mkuu wa baraza la mitihani Dkt.Charles Msonde, halmashauri ya mji Kibaha yenye shule za sekondari 40, kati yake 15 zikimilikwa na serikali na 25 watu binafsi imeendelea kufanya vema huku ikipanda kwa ufaulu ukilinganisha na matokeo ya mwaka, 2019.

Katika mtihani wa kidato cha nne uliofanywa kuanzia mwezi Novemba na kutamatishwa Disemba, 2020, jumla ya watahiniwa 2,588 waliofanya mtihani, 463 wamepata daraja la I, 401 daraja la II, 410 daraja la III, 1149 daraja la IV na 192 hawakufanya vizuri. Aidha, ufaulu umeongezeka kwa asilimia 4.83 kutoka 87.75 mwaka, 2019 mpaka 92.58 mwaka, 2020 huku halmashauri ya mji Kibaha ikifanikiwa kushika nafasi ya nane (8) kitaifa kati ya halmashauri 185 nchini.

Kwa upande wa matokeo ya upimaji wa taifa kidato cha pili, watahiniwa 3,735 walifanya mtihani. Kati ya watahiniwa hao 872 wamepata daraja la I, 396 daraja la II, 484 daraja la III, 1,785 daraja la IV na 195 hawakufanya vizuri. Ufaulu umeongezeka kwa asilimia 1.3 kutoka 93.4 mwaka, 2019 na kufikia 94.7 mwaka, 2020.

Kwa upande wa elimu ya msingi, katika mtihani wa darasa la VII uliofanywa Oktoba, 2020 halmashauri ya mji Kibaha yenye shule 55 ilikua na watahiniwa 3,986 kati yao watahiniwa 3,769 sawa na asilimia 94.6 wamefaulu huku watahiniwa 217 sawa na asilimia 5.4 wameshindwa kufikia wastani wa ufaulu. Hata hivyo, ufaulu umeongezeka kwa asilimia 4.38 kutoka 90.22 mwaka, 2019 na halmashauri imeshika nafasi ya 21 kati ya halmashauri 185 kitaifa.

Aidha, katika mtihani wa darasa la IV uliofanywa Novemba, 2020 kwa kuhusisha shule 60 halmashauri ilikua na watahiniwa 5,239 kati yao watahiniwa 5,223 wamefaulu kwa asilimia 99.69 na watahiniwa 16 sawa na asilimia 0.31 wameshindwa kufikia wastani wa ufaulu. Hata hivyo, ufaulu umeongezeka kwa asilimia 1.44 kutoka asilimia 98.25 mwaka, 2019. Aidha, Kibaha mji imeshika nafasi ya nne (4) kitaifa kati ya halmashauri 185 nchini

Matokeo haya chanya yametokana na uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya elimu unaofanywa na serikali ya jamhuri ya muungano wa Tanzania chini ya Rais wetu Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, usimamizi thabiti wa wasaidizi wake, hamasa toka kwa wadau wa elimu na ari ya walimu katika kutimiza majukumu yao ya msingi.

Innocent J. Byarugaba
OFISA MAWASILIANO, HABARI NA UHUSIANO
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA